

**HATI YA MAKUBALIANO YA KIKAO CHA PAMOJA KATI YA BARAZA LA
BIASHARA LA WILAYA NA BARAZA LA MADIWANI CHA TAREHE 9/02/2018**

Madiwani wa Wilaya ya Mpwapwa wakiongozwa na Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa na wajumbe wa Baraza la biashara la Wilaya chini ya Mwenyekiti wa Baraza ambao pia ni Mkuu wa Wilaya ya Mpwapwa katika kikao cha pamoja kilichofanyika tarehe 9/02/2018 kwa kauli moja wamekubaliana kuwa kwa vile madhumuni ya Baraza la Biashara Wilaya ni kuwezesha kuwepo kwa mazingira bora na rafiki ya kibiashara, na kwa vile kuwepo kwa hali hiyo kutainufaisha Halmashauri, kuanzia tarehe 9/02/2018 Baraza la Madiwani litashirikiana na Baraza la Biashara la Wilaya kuhakikisha kuwa madhumuni ya kuwepo kwa Baraza la Biashara la Wilaya yanafikiwa na kwamba katika kufanya hivyo mambo yafuatayo yatazingitiwa:

1. Mapendekezo yote ya Mkutano wa Baraza la Biashara yaliyowasilishwa katika kikao cha pamoja cha tarehe 9/02/2018 yaandaliwe na kuwasilishwa kwenye vikao vya Halmashauri. Jukumu hilo lifanywe na katibu wa Baraza la Biashara la Wilaya.
2. Wenyeviti wa kamati za kudumu za Halmashauri wawe waalikwa katika Mkutano wa Baraza la Biashara la Wilaya wakati linapojadili masuala yanayohusu sekta za Kamati wanazoongoza.
3. Maamuzi na Mapendekezo ya Mkutano wa Baraza la Biashara la Wilaya yanayohitaji kuhidhinishwa na Baraza la Madiwani yawe yanawasilishwa katika vikao vya Halmashauri. Maamuzi mengine yasiyohitaji kuhidhinishwa na vikao vya Halmashauri yawasilishwe kama taarifa ili kujenga ufahami wa pamoja.
4. Halmashauri itahakikisha kuwa Baraza la Biashara la Wilaya linakuwa na vyanzo madhubuti vya mapato yatakayowezesha Baraza kujiendesha baada ya mradi wa LIC kumaliza muda wake.
5. Kikao cha pamoja kati ya Baraza la Biashara la Wilaya na Waheshimiwa Madiwani kiwe kinafanyika mara moja kila mwaka septemba kabla ya maandalizi ya Bajeti ya Serikali kuanza

.....
Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya
Mpwapwa.

.....
Mwenyekiti wa Baraza la Biashara
Mpwapwa.